

KANUNI NA TARATIBU ZA KILIMO BORA CHA ZAO LA CHOROKO.

Zao la choroko

Utangulizi

Zipo aina mbili za choroko ambazo ni Imara na Nuru hukomaa kwa muda wa siku 55-65. Aidha imara ni nene kuliko nuru lakini nuru inang'ara zaidi ya imara.

Utayarishaji wa shamba

Shamba ni budi litayarishwe mapema kwa mujibu wa kalenda ya kilimo na pia litifuliwe kwa kina cha wastani

Upandaji

Miezi miwili kabla ya mvua kumalizika. Zinaweza kupandwa wakati wa vuli na masika.

Nafasi ya kupanda

Sentimeta 50 kutoka mstari hadi mstari na sentimeta 10 kutoka shina hadi shina

Dhibiti ya wadudu

Zuia wadudu kwa kupulizia dawa mojawapo kati ya Thiordan, Decis, Ripcord au karate mara mbili kuanzia wakati wa kutoa maua na siku saba baadaye. Kama kuna vifuruzi, weka dawa aina ya marshal kwenye mbegu kabla ya kupanda.

Kuvuna na kuhifadhi

Choroko zivunwe wakati zimekauka vizuri kabla ya vitumba kuanza kupasuka. Vuna kwa kuchuma vumba au kung'oa mashina kama vitumba vyote vimekauka. Kuanika juani kisha piga na fito peta anika juani zikauke vizuri kisha hifadhi ghalani. Choroko hubanguliwa haraka kwa hiyo tumia dawa aina ya Acetlic super dust kuzuia wadudu ghalani.

Kiasi cha mavuno

Shamba liliyotunzwa vizuri hutoa magunia magunia 6 hadi 7 kwa ekari moja au kilo 1500-1800 kwa hekta.